**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

*Tele:* +255 026 2322761-5
*Fax No.* +255 026 2322624
**E-mail**: cna@bunge.go.tz

Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S.L.P. 941,
40490 Tambukareli,
**DODOMA.**

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mkutano wa Tatu (3) wa Bunge la 13, umeanza leo Jumanne tarehe 31 Machi, 2026 Jijini Dodoma. Mkutano huu ni mahsusi kwa ajili ya kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara zote kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Shughuli nyingine zitakazofanyika katika Mkutano huo ni kama ifuatavyo:-

### 1.0 KIAPO CHA UAMINIFU NA AHADI YA UZALENDO

Kutakuwa na Kiapo cha Uaminifu na Ahadi ya Uzalendo kwa Waheshimiwa Wabunge Wateule 6 ambao ambao ni:-

a) Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed - Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi;

b) Mhe. Maryam Said Khamis - Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi;

c) Mhe. Said Ali Mbarouk - Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi;

d) Mhe. Shaame Ali Ali - Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi;

e) Mhe. Simai Mohammed Said - Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi; na

f) Mhe. Dkt. Lazaro Killiani Komba - Mbunge Mteule wa Jimbo la Peramiho.

### 2.0 MISWADA YA SERIKALI

Katika Mkutano huu wa Bunge, jumla ya Miswada minne itawasilishwa Bungeni ambayo ni:-

(a) Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2026 (*The Appropriation Bill, 2026*) utapitishwa kwa hatua zote;

(b) Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2026 *(The Finance Bill, 2026)*;

(c) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2026];* na

(d) Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali zinazohamishika wa Mwaka 2026.

**3.0 MASWALI**

Katika Mkutano huu jumla ya maswali ya kawaida 845 yanatarajiwa kuulizwa na kujibiwa Bungeni. Aidha, wastani wa maswali 104 ya papo kwa papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu yataulizwa na kujibiwa siku za Alhamisi.

**4.0 UCHAGUZI WA WABUNGE WA BUNGE LA AFRIKA MASHARIKI**

Kutakuwa na Uchaguzi wa Wabunge wawili wa Bunge la Afrika Mashariki kuziba nafasi zilizowazi baada ya Mheshimiwa James Kinyasi Millya na Mheshimiwa Dkt. Ngwaru Jumanne Maghembe kuchaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025. Tangazo la Uchaguzi huo litatangazwa kwenye Gazeti la Serikali na tarehe ya Uchaguzi huo itatolewa rasmi baada ya taratibu zote kukamilika.

Ratiba yote ya Shughuli za Mkutano wa Tatu (3) wa Bunge inapatikana katika Tovuti ya Bunge ambayo ni www.bunge.go.tz.

**Imetolewa na**: Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma,
Ofisi ya Bunge,
**DODOMA.**

31 Machi, 2026.